

Learning by Ear

"Everyone's Different – Respect for Minorities"

Episode 10:

Dance with Us – Africans in Germany

Author: Marta Barroso

Editor: Katrin Ogunsade, Adrian Kriesch

Proofreader: Charlotte Collins

Characters

<i>Narrator</i>	m'mke	Umiri kiasi miaka 30	english
<i>Yahi Nestor Gahe</i>	m'mume	32	german
<i>Steve Bimamisa</i>	m'mume	Umiri kiasi miaka 30	german
<i>Study quotation</i>	male/m'mke	?	english?
<i>Clip Actor</i>	m'mume	Umiri kiasi miaka 30	german

Intro:

Hujambo na karibu kwenye kipindi chetu cha **“Noa Bongo Jenga Maisha Yako”**. Hii ni sehemu yetu ya kumi na ya mwisho ya mfululizo wetu wa **“Kila mtu ni tofauti- Kujali maslahi ya jamii za walio wachache”**. Visa vyetu kutoka maeneo mbalimbali barani vimekukutanisha na watu wanaokabiliana na ubaguzi. Katika kipindi cha leo, tunakutana na Nestor na Steve. Wote wawili wanatoka Afrika na wanaishi Ujerumani ambapo wanatangaza kuvumiliana na jinsi ya kujumuisha jamii za walio wachache nchini humo. Hayo ndio maudhui ya muziki wa bendi yao, Diversité: kuishi pamoja, badala ya kuishi kando kando.

1. SFX Drinking tea, theatre entrance hall, stays loud, then fade under

2. Narrator:

Yahi Nestor Gahe atajibwaga jukwaani kiasi ya saa moja unusu ijayo, lakini hana wasiwasi. Kijana huyo ameketi katika ukumbi wa “tri-bühne”, ukumbi wa michezo ya kuigiza katika mji wa Stuttgart nchini Ujerumani, ambapo hufanya kazi ya uigizaji, upangaji miondoko ya ngoma na uchezaji ngoma. Anakunywa chai yake taratibu huku akila

soga na rafiki yake Steve Bimamisa. Wanatumia muda huo kuzungumia mradi wao mpya. Mradi huo unatarajiwa kuzinduliwa kiasi miezi miwili ijayo katika ukumbi huo. Steve anasubiri kwa hamu kwa tumbuizo jipya.

3. SFX Schuhplattler/Gumboot (NOT live), fade in under text above, stays loud, then fade under

4. Clip Steve (german):

“Tumejumuisha ngoma kutoka Afrika Kusini na ngomani kutoka Bavaria. Nestor anaanza kwa ngoma ya “Gumboot” kutoka Afrika Kusini kisha anaingia kwenye ngoma ya “Schuhplattler” ya Bavaria.”

5. SFX Schuhplattler/Gumboot (NOT live), gets loud again, then fade under, then long fade out under following text

6. Narrator:

Wanaume waliokuwa wakifanya kazi katika migodi ya dhahabu nchini Afrika Kusini hawakuwa na budi kuvaa mabuti ya mpira ya Wellingto ambayo wenyewe wanayaita, ‘gumboots’. Serikali ya ubaguzi wa rangi ilikuwa imepiga marufuku upigaji ngoma. Wachimba migodi weusi wakaanza kutumia mabuti yao kuwasiliana kwenye migodi yenye giza na baadaye wakawa na midundo tofauti tofauti.

‘Schuhplattler’ nayo ni ngoma ya kienyeji wa eneo la Bavaria, Ujerumani kusini. Vijana wa kiume walianzisha ngoma hiyo kuwakitumbuiza wasichana waliokuwa wametimia umri wa kuolewa. Kwenye ngoma hiyo, walivaa “Lederhosen”, suruali za kienyeji za ngozi za Bavaria.

Ingawa ngoma hizo zilianzia maeneo tofauti, wanamuziki hao wanashangazwa na jinsi zinavyofanana. Onyesho hilo la “Gumboot-Schuhplattler” la bendi ya Nestor na Steve tayari limekuwa kivutio kikubwa. Kundi hilo linaitwa Diversité, na muziki wao ni– kama wasemavyo wenye bendi – aina mpya ya muziki unaochanganya aina nyingi za miziki. Kulingana na Nestor, Diversité - or, katika Kiingereza, ‘diversity’ - ni neno lililo na maana zaidi ya kuwa na mambo tofauti tofauti.

7. Clip Nestor (german):

“Diversity’ ni ile hali ya uanuwai maanake vitu ambavyo si sawa lakini vinaweza kujumuishwa. ‘Diversity’ – Diversité – ni kwamba kila mmoja wetu ni tofauti na mwenzake. Lakini tukiungana tunaweza kuafikia mambo makubwa.”

8. Narrator:

Bendi ya Diversité inawajumuisha wasanii kutoka Afrika na Ujarumani. Wao hutumbuiza kwa makundi tofauti

kutegemea onyesho lililokusudiwa lakini wasanii wakuu ni Nestor, Steve, na Michael Dikizeyek ambaye ni muimbaji na mtunzi wa nyimbo. Wote wanasema kwamba muziki na ngoma ndio njia mwafaka ya kuwaunganisha watu. Kulingana na Steve hiyo ndiyo njia mwafaka ya kuelezea fikra yake ya umoja kwenye huo uanuwai.

9. Clip Steve (german):

“Kuwaonyesha watu: ‘mnadhani kwamba sisi ni tofauti na nyinyi, lakini tazameni: ingawa sisi ni weusi, tunacheza ngoma ya Schuhplattler!’”

10. Narrator:

Steve amelelewa kwa kiasi fulani nchini Ujeruamani. Aliwasili pamoja na familia yake nchini humu kiasi miaka 16 iliyopita na alihudhuria shule karibu na Stuttgart. Ana umri kiasi miaka 30 ingawa hasemi umri wake. Steve ni mjasiriamali: nimekuwa msimamizi wa kampuni ya muziki kwa kiasi miaka sita iliyopita na tangu mwaka 2009 amekuwa mtayarishaji wa muziki wa bendi ya Diversité. Kulingana naye, nchi ya Ujerumani imo katika harakati ya kujikurubisha zaidi kwenye maeneo mengi ya ulimwengu na pia kwa wahamiaji.

11. Clip Steve (german):

“Kati ya mwaka wa 1998 na 2000, ilikuwa vigumu sana kwa familia ya Kiafrika kupata nyumba ya makazi. Hakuna aliyekubali kutupatia vyumba. Wenyeji walikuwa wakitudanganya kwamba vyumba vya tayari vina wapangaji. Na saa mbili baadaye familia nyingine ingekodishiwa vyumba hivyo hivyo. Wakati huo nilikuwa skauti na nilikuwa nikija Stuttgart mara kwa mara. Polisi walikuwa wakiwachunguza Waafrika pekee katika vituo vya magari moshi. Sasa hivi mambo yamebadilika.”

12. Narrator:

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2009 uliodhaminiwa na Wakala wa Muungano wa Ulaya kuhusu Haki za Kimsingi, watu wa jamii ya Waroma, wanaojulikana zaidi kwa jina “gypsies” ndio jamii ambayo imeathiriwa zaidi na ubaguzi katika mataifa ya Umoja wa Ulaya, wakifuatiwa na wahamiaji wanaotoka Afrika, kusini mwa Jangwa la Sahara. Kulingana na utafiti huo:

13. Clip quotation:

“Makundi kumi yanayoongoza kwenye orodha ya kubaguliwa kwa kiasi cha miezi kumi ni: Waroma katika Jamhuri ya Cheki, Waafrika nchini Malta, Waroma nchini Hungary, Waroma nchini Poland, Waroma nchini Ugiriki,

raia wa Afrika, kusini mwa jangwa la Sahara nchini Ireland, raia wa Afrika Kaskazini nchini Italia, Wasomali nchini Finland, Wasomali nchini Denmark, na raia wa Brazil nchini Ureno.”

14. SFX Nestor talking to Steve, then fade under

15. Narrator:

Hata hivyo, harakati za kujumuisha tamaduni mbalimbali zina changamoto zake. Bendi hiyo ililazimika kuwanunulia wachezaji “Lederhosen” kadhaa. Suruali za awali zilikuwa ndefu zaidi, na za mara ya pili zikawa zinawazuia kucheza vizuri. Iliwabidi wachezaji hao kujifunza kwa kina ngoma hiyo ya Bavaria, kuirekebisha kidogo na kufanya mazoezi makali.

16. Clip Steve (german):

“Tunadhani huku kutangamana ni suala la kuchagiza. Kwa wachezaji, pia. Tumeshuhudia mapaja yao yakiwa na rangi ya samawati kwa sababu mtu huyapiga makofi anapocheza Schuhplattler. Ni jambo la kuvutia unapoona ugumu uliopo

mtu anapojifunza jambo jipya. Kuishi na binadamu wenzio ni kazi; inahitaji uvumilivu mwingi.”

17. Narrator:

Kwa mujibu wa Ofisi ya Uhamiaji na Wakimbizi ya Ujerumani, takriban wahamiaji milioni saba walikuwa wakiishi Ujerumani mwaka 2010. Katika eneo la Baden-Württemberg ambako Nestor na Steve wanaishi, asilimia kumi na moja ya wakazi wake ni wahamiaji. Hata hivyo, utafiti wa mwaka 2009 wa Wakala wa Muungano wa Ulaya wa Haki ya Kimsingi ulizingatia sera ya Ujerumani ya kutangamanisha wakazi kuwa sera inayoafiki. Kwa sababu hiyo nchi ya Ujerumani haimo miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa ubaguzi katika mataifa ya Muungano wa Ulaya.

18. SFX Music playing, Nestor singing to music, then fade under

19. Narrator:

Nestor aliwasili nchini Ujerumani mwaka 2005. Aliondoka nchini mwake, Ivory Coast, Afrika Magharibi, ili afanye kazi ya upangaji wa miondoko ya ngoma na pia uchezaji ngoma katika tamasha lililoendeshwa kote nchini kwa muda wa

miaka mitatu. Muda wa kibali chake cha kazi ulipomalizika mnamo mwaka 2008, alikuja mjini Stuttgart. Tayari ameshaoa mke wa Kijerumani na sasa hana mipango ya kurudi nyumbani. Anakiri kwamba kuna ubaguzi; lakini hapa Ujerumani Magharibi ubaguzi haujitokezi waziwazi:

20. Clip Nestor (german):

“Napenda sana kutembea jioni mimi na mke wangu. Lakini katika baadhi ya baa na migahawa Waaafrika huwa wachache. Kwa hivyo, kila mtu anatutumbulia macho. Wakati wote! Wao hunitazama kwa kuwa ninaonekana tofauti, rangi ya ngozi yangu ni tofauti. Bahati ni kwamba hapa hawaonyeshi moja kwa moja, utawajua tu jinsi wanavyokutazama.”

21. Narrator:

Nestor hapendi kutazamwa hivyo. Lakini hali hubadilika anapokuwa jukwaani. Sasa ni wakati wa Nestor kupanda jukwaani. Onyesho la leo jioni kiasi dakika kumi zijazo. Usiku huu Nestor hahitajiwi kuvaa mavazi ya kuingia jukwaani.

22. SFX People entering auditorium, actor speaking, long fade in

23. Clip Actor (german):

“Wapendwa watazamaji, kwanza kabisa ningependa kuwashukuru nyote kwa kuhudhuria ...” **long fade out**

24. Narrator:

Steve tayari ameshamuona Nestor akiigiza, lakini anataka kutumia fursa hiyo kuuchunguza ukumbi. Anataraji pia kutumbuiza na wenzake wa bendi ya Diversité wakati wa kuzinduliwa **mchanganyiko wa ngoma mbili** “Gumboot” na “Schuhplatteln” kiasi ya miezi miwili ijayo. Ni ukumbi mdogo; anapenda wakati watazamaji wanapokaa karibu na bendi ili apate kuzitazama nyuso zao moja kwa moja.

25. SFX Nestor dancing to music, begins under text above, then gets loud, then long fade out under next text

26. Narrator:

Onyesho linachukua muda wa saa moja bila mapumziko. Watazamaji wametumbuizwa si haba! Hata waigizaji wengine wanaisifu ngoma ya Nestor.

27. SFX People clapping, begins under text above, stays loud, then long fade out under next text

28. Narrator:

Takriban miezi miwili hivi ijayo, atacheza ngoma hapa kwa mara nyingine, lakini mara hii pamoja na bendi ya Diversité. Kisha yeye, Steve na wachezaji wengine wa bendi watakuwa na maonyesho ya kila mwezi kueneza ujumbe wao: kwamba watu wanapaswa kuishi pamoja, wala si kando kando.

29. SFX Diversité, then long fade out (NOT live)

Outro:

Na huo ndio mwisho wa kipindi cha leo. Hii ilikuwa sehemu ya mwisho ya kipindi chetu cha “**Noa Bongo Jenga Maisha Yako**” kuhusu kuzingatia maslahi ya jamii za walio wachache. Sehemu hii imeandikwa na Marta Barroso. Ukitaka kusikiliza tena sehemu hii au sehemu nyingine za vipindi vyetu vya “**Noa Bongo Jenga Maisha Yako**” tazama ukurasa wetu wa wavuti www.dw.de/lbe. Tunakushukuru kwa kuwa nasi. Kila la kheri.